Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU *Bulletin*

*JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.26 - 2023*




wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaendelea kuboresha Elimu yetu*


## Toleo MAALUM



# MIAKA MIWILI YA MAGEUZI, KUONGEZA FURSA KATIKA SEKTA YA ELIMU

## - KAZI IENDELEE -

ToleoMAALUM >



# MIAKA MIWILI YA MAGEUZI NA KUONGEZA FURSA KATIKA SEKTA YA ELIMU, KAMPASI MPYA 14 ZINAJENGWA KATIKA MIKOA 14

RAIS Samia Suluhu Hassan wakati wa kulihutubia Bunge aliweka bayana dhamira ya Serikali yake ya kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na kufanya mabadiliko ya Mitaala iliyopo ili ielekezwe kwenye kutoa elimu ujuzi kulingana na mahitaji ya soko Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia kumeshuhudiwa maboresho makubwa katika sekta ya elimu na utekelezaji wa kazi kulingana na azma yake ya kuhakikisha elimu inakuwa ni kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa kutoa wahitimu wenye ujuzi na stadi.

Akizungumza katika nyakati mbalimbali, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda alisema, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kukuza na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu katika ngazi zote za elimu na kuhamasisha kuendeleza teknolojia na ubunifu wa ndani ikiwa ni pamoja kuzibiasharisha.

Alisema Wizara imeweza kutekeleza kazi kubwa ya kufanya mabadiliko ya mitaala ya elimu na Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na kuwa rasimu za Mitaala hiyo ya elimu msingi na sera muda si mrefu itatolewa kwa wananchi kwa ajili ya kupata maoni ya mwisho.

"Pia mapitio ya mitaala kwa ngazi ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi pamoja na Elimu ya Juu yanaendelea kwa lengo la kuhakikisha elimu inayotolewa ni bora na inawajengea wahitimu kuwa na ujuzi na maarifa yatakayowapatia stadi zitakazowawezesha kushiriki katika shughuli za kiuchumi kitaifa na kimataifa"



baadhi ya mafundi waungaji vyuma wakiwa kwenye mafunzo ya muda mfupi ya ujuzi yanayotolewa na vyuo vya maendeleo ya wananchi (FDC) nchini

Kwa upande wa Elimu ya Juu, Profesa Mkenda alisema Serikali imeendelea kuhakikisha wanafunzi wa Elimu ya Juu wanasoma katika mazingira rafiki na wezeshi. Serikali ya Awamu ya Sita imelenga kukuza uchumi na kuboresha huduma za kijamii kama elimu kwa uwiano sawia katika mikoa na maeneo yote.

Alisema Serikali ilitafuta na kupata mkopo wa Sh bilioni

# Toleo**MAALUM** >

972 wenye riba nafuu kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), lengo likiwa ni kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vikuu pamoja na kuongeza kampasi zaidi.

Kupitia mradi wa HEET, zitajengwa Kampasi 14 mpya za vyuo vikuu katika mikoa ambayo haina vyuo vikuu ikiwemo ya Kigoma, Ruvuma, Singida, Buyu Zanzibar, Kagera, Tanga, Mwanza, Tabora, Manyara, Simiyu, Shinyanga, Lindi, Rukwa, na Katavi.

Kupitia mradi huo pia yatajengwa mabweni 34; vyumba vya mihadhara na madarasa 130; kumbi za mikutano ya kisayansi 23; maabara/karakana za kufundishia 108; miundombinu ya shambani na vituo atamizi 10 hatua ambayo itasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma programu za kipaumbele ambazo ni Sayansi, Teknolojia, uhandisi na Hesabu (STEM) kutoka wanafunzi 40, 000 kwa mwaka 2020 hadi kufikia 106,000 mwaka 2026.

Pia utaboresha mitaala ya programu za kipaumbele cha Taifa kwa kuhuisha na kuandaa mitaala mipya zaidi ya 290, kusomesha Wahadhiri 387 na Wahadhiri 3,500 wanatarajiwa kupata mafunzo kwa vitendo viwandani ifikapo mwaka 2026.

Kwa upande wa kuongeza fursa za elimu, bajeti ya fedha za mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka Sh bilioni 570 katika mwaka wa fedha 2021/22 hadi kufikia bilioni 654 mwaka 2022/23 hivyo kufanya jumla ya wanufaika kuongezeka kutoka wanafunzi 177,892 mwaka 2020/21 hadi wanafunzi 202,877 kwa mwaka 2022/23. Alisema pia Serikali iliondoa tozo ya asilimia 6 ya kulinda thamani ya fedha katika urejeshaji wa mkopo na tozo ya adhabu ya asilimia 10 ya mkopo wanayotozwa wanufaika.

Pia kumekuwa na ongezeko la udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka 87,934 mwaka 2020/21 hadi 106,620 mwaka 2021/22, na mwaka 2022/2023 udahili umefikia 113, 383.

2 MIAKA MIWILI YA MAMA KAZINI



Taasisi ya Sayansi za Bahari Buyu Zanzibar

# Toleo**MAALUM** >

"Mwaka 2022/23 Serikali pia imeanzisha mpango wa kusomesha wanafunzi wenye ufaulu wa juu wa Kidato cha Sita katika masomo ya Sayansi ambayo ni moja ya kipaumbele cha Taifa kupitia Mpango wa 'Samia Scholarship' na jumla ya shilingi bilioni 3 zimetengwa ambapo wanafunzi 640 wamenufaika na ufadhili huu ambao wamedahiliwa katika vyuo mbalimbali nchini"

Profesa Mkenda alisema katika kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi stadi, Serikali imetumia kiasi cha Sh bilioni 30.84 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya 25 kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19.

2 MIAKA MIWILI YA MAMA KAZINI

Katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuwa na chuo cha VETA cha Wilaya katika kila Wilaya na katika kila Mkoa, imetenga Shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kuwezesha kuanza ujenzi wa Vyuo 64 vya VETA ngazi ya Wilaya katika Wilaya ambazo hazina vyuo vya ngazi hiyo pamoja na kuanza kwa ujenzi wa Chuo cha VETA ngazi ya Mkoa katika Mkoa wa Songwe ambao hauna chuo katika ngazi hiyo.

Serikali pia inakamilisha ujenzi wa Chuo kipya cha kisasa cha Ufundi Dodoma kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 17 kwa awamu ya kwanza ambapo kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kudahili Wanafunzi 1,500 kwa mara moja. Chuo hiki kikikamilika kabisa kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi zaidi ya 3,000.

Katika kuboresha Mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo vya Ualimu, Serikali imetumia Shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi, upanuzi na ukarabati wa vyuo vinne na kukarabati vingine 27, hatua ambayo itaongeza udahili kutoka 17,000 hadi kufikia zaidi ya 22,000. Katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwenye ufundishaji na ujifunzaji, Serikali imegawa vishkwambi kwa Walimu wote wa shule za umma Tanzania Bara na Zanzibar. Vile vile wakufunzi wote wa Vyuo vya Ualimu na VETA, Vyuo vya Maendeleo vya Wananchi (FDCs) na wathibiti Ubora wa Shule wamepatiwa vishkwambi hivyo ili kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji. Jumla ya vishkwambi 285,451 vimegawiwa kwa makundi hayo.



Ugawaji Vishkwambi kwa walimu wa Shule za Umma nchini




Wanafunzi wakionesha vitabu vya kiada

# Toleo**MAALUM** >

Alisema pia Serikali imejenga Shule ya Mfano ya Sekondari iliyopo Iyumbu jijini Dodoma kwa gharama ya zaidi ya Shilingi bilioni 17 ambayo ikikamilika itakuwa na uwezo wa kuchukua Wanafunzi 1000 kwa wakati mmoja, Ujenzi wa Shule ya Msingi ya Mfano jumuishi Lukuledi kwa gharama ya zaidi ya Shilingi bilioni moja ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 320 kwa wakati mmoja na Ujenzi wa Shule ya Mfano jumuishi ya Awali, Msingi, Sekondari ya Mbuye iliyopo Chato kwa gharama ya zaidi ya Shilingi bilioni nne na itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 680 kwa wakati mmoja, lengo ni kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu iliyo bora katika mazingira salama kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.



**Shule ya Sekondari ya Mfano inayojengwa Iyumbu Dodoma**

Alisema katika sekta ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, tumeona namna Serikali ilivyofanikiwa kuibua Wabunifu wapatao 1,581 ambapo kati yao 153 wametambuliwa na 27 wameendelezwa na 9 kati yao wamefikia katika hatua ya kubiasharisha tafiti zao. Lakini katika kipindi hiki cha miaka miwili tumeona Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu yakipelekwa mpaka katika ngazi ya wilaya, lengo likiwa ni kuwapata wabunifu waliopo chini na kukuza ubunifu na Teknolojia zinazozalishwa.

2 MIAKA MIWILI YA MAMA KAZINI



**Mbunifu akiwa katika kitimwendo alichobuni kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum**

# Toleo**MAALUM** >

Shule ya msingi ya mfano Lukuledi



Kupitia Mradi wa SEQUIP Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imejenga Shule 232 za Sekondari na Shule za Sekondari za wasichana za Sayansi katika mikao 10 ambapo lengo ni kujenga shule hizo katika kila mkoa ili kusogeza fursa za watoto kusoma sayansi karibu na mazingira yao.

2 MIAKA MIWILI YA MAMA KAZINI

"Moja ya eneo kubwa la kujivunia ni Serikali kutoa fursa ya wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito kurejea shule ambapo hadi kufikia Januari, 2023 wanafunzi zaidi ya 4,933 wamerejea shule, hili pia limetokea katika kipindi cha miaka miwili ya Mhe. Rais Samia."

Alisema Serikali ya awamu ya sita imeazimia na inahakikisha kila mtoto bila kujali hali ya ulemavu anapata fursa ya kupata elimu bila vikwazo, Serikali imenunua vifaa wezeshi na malipo ya bima za afya kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa gharama ya Shilingi milioni 664.

Chuo cha Ufundi kinajojengwa Dodoma



Chuo cha VETA Kagera



# Toleo**MAALUM** >

Pia imenunua vishkwambi (Tablets) 330 kwa ajili ya wanafunzi viziwi vyenye gharama ya Shilingi milioni 134 kwa ajili ya shule 15 za msingi zinazopokea wanafunzi viziwi. Pia Serikali menunua vitimwendo 1,334 vyenye thamani ya Shilingi milioni 191 kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa viungo waliobainika kuwa na uhitaji katika shule za msingi na sekondari.



Mafunzo ya ufundi na ujuzi



Ukarabati wa vyuo vya ualimu vya umma

Ubora wa elimu unaendana na uwepo wa mifumo sahihi, nguvu kazi na vitendea kazi kwa ajili ya usimamizi na uthibiti ubora wa Elimu. Katika pindi cha miaka miwili ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali imenunua na kusambaza magari 38 kwa ajili ya ofisi za uthibiti ubora wa shule kwa lengo la kuimarisha uthibiti wa elimu nchini. Sambamba na hilo, Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 2.6 kwa kuimarisha ufuatiliaji wa ufundishaji shuleni na kuwawezesha Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule kutoa ushauri kwa lengo la kuboresha elimu.

2 MIAKA MIWILI YA MAMA KAZINI

"Wizara inajivunia na kushukuru maono na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais Samia na kumshukuru kwa kuendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya Elimu.

## NUKUU > TUTAJIELEKEZA KATIKA KUFANYA MAPITIO YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 NA KUFANYA MAREKEBISHO KWENYE MITAALA ILIYOPO ILI IELEKEZWE KWENYE KUTOA ELIMU UJUZI KULINGANA NA MAZINGIRA YA NCHI NA SOKO LA AJIRA

***– Mhe. Samia Suluhu Hassan,***
***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***
***Bungeni - April, 2021***

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

---

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

---

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifala Elimu ya Ufundi (NACTE),**
S.L.P 7109, DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

---

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P. 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

---

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

---

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

---

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

---

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

---

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz